SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.17 December 2025

MITAZAMO YA WATUMIAJI WA BIDHAA JUU YA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA VIFUNGASHIO VYA BIDHAA

Twaiba A. Omar
thuwaibaomar2021@gmail.com
Department of Swahili,
School of Swahili and Foreign Languages,
Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA

Received: September 2025, Accepted: Novembre 2025, Published: December 2025
© SUMAIT University Journal 2025

Abstract:
This article examines consumers' perceptions of the use of languages on food product packaging. The data for this article were obtained through interviews. The research sample consisted of 30 product consumers living in different areas within the Urban District. The theory of language planning orientations initiated by [20] was used in analyzing the data for this article. This theory is based on three principles, all of which were fully applied in the data analysis. These principles are language as a problem, language as a right, and language as a resource. The findings revealed that food product consumers in Zanzibar hold both similar and differing views depending on their arguments. The perceptions that emerged were as follows: (1) Kiswahili must be used on product packaging; (2) product packaging should use both Kiswahili and foreign languages; and (3) foreign languages should not be used at all on the packaging of products produced and sold in Tanzania. Most of the respondents agreed with the view that Kiswahili and international languages should be combined. Based on these findings, I recommend that the relevant authorities take appropriate measures to ensure that product packaging combines Kiswahili with foreign languages particularly English and Arabic. Such a step would help meet the needs of a larger number of consumers.

Ikisiri*:*

Makala hii imechunguza mitazamo ya watumiaji wa bidhaa za chakula juu ya matumizi ya lugha za vifungashio vya bidhaa. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano. Sampuli ya utafiti huu ni watumiaji 30 wa bidhaa za chakula ambao wanaishi Wilaya ya Mjini kutoka maeneo tofauti. Nadharia ya Mielekeo ya Upangaji wa Lugha iliyoasisiwa na [20] ndio iliyotumika katika uchambuzi wa data za makala hii. Nadharia hii ina misingi mitatu ambayo yote imetumika kikamilifu katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Misingi hiyo ni: Lugha kama tatizo, lugha kama haki na lugha kama rasilimali. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa watumiaji wa

bidhaa za chakula Zanzibar wana mitazamo inayofanana na kutofautiana kulingana na hoja zao. Mitazamo hiyo ilijitokeza kama ifuatavyo: Kiswahili lazima kitumike katika vifungashio vya bidhaa, vifungashio vya bidhaa vitumie lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni na mtazamo wa mwisho ni ule unaoamini kuwa lugha za kigeni hazipaswi kutumika katika vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa Tanzania na kuuzwa Tanzania. Watumiaji wengi waliohojiwa wamekubaliana na mtazamo wa kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni. Kutokana na matokeo haya makala hii inapendekeza kwa mamlaka husika ichukue hatua stahiki ili kuhakikisha vifungashio vya bidhaa vinachanganya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni hususan Kiingereza na Kiarabu. Hatua ambayo itasaidia kukidhi haja ya watumiaji walio wengi zaidi.

Keywords: Mitazamo, Vifungashio, Bidhaa, Chakula, Jamii

1.0 Utangulizi

Makala hii inahusu mitazamo ya watumiaji wa bidhaa juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula zilizopo Zanzibar. Vifungashio vya bidhaa zilizopo Zanzibar hutumia lugha mbalimbali kama vile Kiswahili, Kiingereza, Kiarabu, Kituruki, Kichina, Kijerumani na Kijapani. Matumizi hayo ya lugha katika vifungashio vya bidhaa, yanatarajiwa kumuwezesha mtumiaji wa bidhaa kufahamu maelekezo mbalimbali yanayohusiana na bidhaa. Maelekezo hayo ni yale yanayohusiana na vipimo, tahadhari, namna ya kuhifadhi bidhaa, namna ya matumizi, muda unaostahiki kutumia bidhaa, viambata vilivyomo katika bidhaa husika na jina la bidhaa. Hali ambayo humuwezesha mtumiaji wa bidhaa kutumia bidhaa kwa uhakika na kujiamini.

Tafiti za awali zinaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la vifungashio vya bidhaa ambazo hutumia lugha za kigeni kuliko lugha ya wazawa, ilhali watumiaji wengi wa bidhaa hizo wanafahamu zaidi lugha yao mama ambayo kwa kawaida huitumia katika harakati zao za maisha [2]. Utumiaji wa lugha za kigeni pekee katika bidhaa ni hatari kwa watumiaji wa bidhaa hizo. Hali hii imemsukuma mtafiti kuchunguza mitazamo ya watumiaji wa bidhaa za chakula Zanzibar juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa.

2.0 **Mbinu na Nadharia ya Utafiti**

Makala hii imetumia mkabala changamani uliofafanua data kwa mbinu ya kitaamuli pamoja na nambari. Mbinu ya kimaudhui imetumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Kwa sababu uchambuzi ulitazama zaidi namna watumiaji wanavyovijadili vifungashio vya bidhaa za chakula. Utafiti huu umefanyika uwandani. Kwa vile huko ndiko wanakopatikana watumiaji wa bidhaa. Mbinu iliyotumika wakati wa ukusanyaji wa data ni mahojiano. Mbinu hii imemuwezesha mtafiti kupata data zinazohusiana na mitazamo ya watumiaji wa bidhaa juu ya lugha zinazotumika katika vifungashio vya bidhaa za chakula Zanzibar. Utafiti huu umejikita katika eneo la Wilaya ya Mjini Zanzibar. Sampuli ya utafiti huu ni watumiaji wa bidhaa thelathini 30 ambao walipatikana kutoka maeneo tofauti ya Wilaya ya Mjini. Maeneo hayo ni kama vile, Mji Mkongwe, Muembeladu, Kikwajuni, Amani na Mpendae. Upatikanaji wa watoa taarifa hao ulitumia usampulishaji wa kieneo.

Aidha, Nadharia ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha iliyoasisiwa na [20] imetumika. Lengo kuu la nadharia hii ni kuchambua mitazamo ya watumiaji wa bidhaa kuhusu matumizi ya lugha za vifungashio. Nadharia hii husaidia kuelewa ni kwa namna gani lugha huweza kuonekana kama changamoto, haki au rasilimali na hivyo kusaidia katika kutoa mapendekezo ya kisera au kiutendaji kulingana na muktadha wa jamii husika.

3.0 Matumizi ya Lugha katika Vifungashio vya Bidhaa za Chakula Zilizopo Zanzibar

Uchambuzi wa data kuhusu mitazamo ya watumiaji wa bidhaa Zanzibar juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula umebaini kuwepo kwa mitazamo mikuu mitatu. Mtazamo wa kwanza, umesisitizaa kuwa lugha ya Kiswahili ni lazima kutumika kwa sababu sio tu ni lugha ya taifa na ya biashara kwa Wazanzibari, lakini pia ni chombo muhimu cha mawasiliano ya wananchi walio wengi. Mtazamo huu unasisitiza matumizi ya lugha Kiswahili katika vifungashio ili kuongeza uelewa na usalama wa watumiaji. Mtazamo wa pili unaunga mkono matumizi ya lugha mbili au zaidi; Kiswahili na Kiingereza au Kiswahili na Kiarabu, kwa lengo la kuwahudumia kwa ufanisi watumiaji wa ndani na wa nje. Mtazamo wa tatu unapinga matumizi ya lugha za kigeni katika vifungashio vya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania na kuuzwa Tanzania, ukieleza kuwa hali hiyo huathiri haki ya lugha ya wazawa, kushusha hadhi ya Kiswahili na kuhatarisha urithi wa kitamaduni wa jamii ya Zanzibar. Jadweli lifuatalo linaonesha kwa muhtasari mgawanyo wa mitazamo hiyo kiasilimia:

Jadweli Na. 1: Mitazamo ya Watumiaji wa bidhaa za chakula kuhusu lugha

Mitazamo ya Watoataarifa	**Idadi**	**Asilimia (%)**
1. Kiswahili ni lazima kitumike	10	33.3%
2. Kiswahili kitumike na lugha nyingine za kigeni	14	46.7%
3. Lugha za kigeni zisitumike	06	20.0%
Jumla	**30**	**100%**

Chanzo: Data ya Utafiti (2024)

Jadweli la hapo juu linaonesha mitazamo ya watumiaji wa bidhaa za chakula kuhusu matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa hizo. Uchambuzi kamili wa mitazamo hiyo ni kama ufuatavyo:

3.1 Kiswahili Lazima Kitumike katika Vifungashio vya Bidhaa

Mtazamo mmoja wapo ni muhimu uliojitokeza katika matokeo ya utafiti huu ni kwamba lugha ya Kiswahili inapaswa kutumika kwa lazima katika vifungashio vya bidhaa zinazouzwa Zanzibar. Mtazamo huu umeungwa mkono na watoataarifa kumi (10) kati ya thelathini (30), sawa na asilimia 33.3 ya washiriki wote wa utafiti. Watoataarifa hawa wameeleza hoja mbalimbali zinazoonesha umuhimu wa kutumia Kiswahili katika vifungashio, wakitambua kuwa ni lugha ya taifa na lugha mama ya Wazanzibari.

Hoja zilizotolewa na watoataarifa zimeainisha nafasi ya Kiswahili kama lugha ya wazawa, lugha ya biashara, pamoja na lugha inayowavutia watumiaji wa kawaida kufuatilia maudhui yaliyomo katika vifungashio. Tazama jadweli lifuatalo linaloonesha mitazamo ya ulazima wa kutumika kiswahili:

Jadweli Na. .2: Mtazamo wa kutumika kwa Kiswahili katika Vifungashio

Hoja za watoataarifa	**Idadi**	**Asilimia**
1. Kiswahili kitumike kwa sababu ni lugha ya wazawa	05	50%
2. Kiswahili kitumike kwa sababu ni lugha ya kibiashara	02	20%
3. Kiswahili kitumike kwa sababu kinajenga shauku ya kusoma vifungashio kwa watumiaji wazawa.	03	30%
Jumla	**10**	**100%**

Chanzo: Data ya Utafiti (2024)

Kwa mujibu wa data hii, asilimia 50 ya watoataarifa wamesisitiza kuwa Kiswahili kinapaswa kutumika kwa sababu ni lugha ya wenyeji wa Zanzibar, asilimia 20 walikitambua kama lugha muhimu ya biashara, huku asilimia 30 wakibainisha kuwa matumizi ya Kiswahili yanachochea shauku na uelewa wa watumiaji wa bidhaa. Maoni haya yanadhihirisha kuwa Kiswahili si tu chombo cha mawasiliano, bali pia ni daraja muhimu linalowaunganisha watumiaji wa bidhaa na taarifa muhimu zinazohusu bidhaa hizo.

3.1.1 Kiswahili Kitumike kwa Sababu ni Lugha ya Wazawa

Hoja nyingine iliyotolewa katika mtazamo huu ni umuhimu wa kutumia Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa zinazouzwa Zanzibar kwa sababu ndio lugha ya wazawa. Watoa taarifa watano kati ya kumi, sawa na asilimia 50, walisisitiza kuwa Kiswahili kina nafasi ya kipekee katika maisha ya Wazanzibari, hivyo lazima kitumike katika vifungashio kwa sababu ni lugha mama ya Wazanzibari. Kwa mtazamo wao, lugha ya Kiswahili ndiyo nyenzo kuu ya mawasiliano na ndiyo inayoeleweka kwa wananchi wengi wa zanzibar. Watoataarifa hao walieleza kuwa, matumizi ya lugha ya kigeni pekee katika vifungashio huwatenga wazawa katika ufahamu sahihi wa taarifa muhimu zinazohusu bidhaa hizo.

Mmoja wa watoataarifa alieleza kwamba:

> "Lugha ya Kiswahili haipaswi kudharauliwa kwa sababu ni rasilimali muhimu na hubeba maisha ya kila siku ya Wazanzibari[1]"

Nukuu hii inaonesha uhusiano wa karibu baina ya lugha na utambulisho wa jamii na inasisitiza kwamba lugha ya Kiswahili ni zaidi ya chombo cha mawasiliano; ni rasilimali ya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi.

[1] *Maelezo haya yametolewa na mtoa taarifa "A" kutoka Mji mkongwe akiwa ni mmoja wa watumiaji wa bidhaa zinazopatikana Zanzibar. Taarifa hii ilitolewa tarehe 23/09/2024.*

Nukuu hii inaendana moja kwa moja na Nadharia ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha iliyoasisiwa na [20] hasa kupitia msingi wake wa lugha kama rasilimali. Kwa mujibu wa msingi huu, lugha inapaswa kuangaliwa kama chombo cha maendeleo chanya, ambacho kinaweza kuimarisha mshikamano wa kijamii, kuongeza ushiriki wa wananchi katika maendeleo na kuchochea usawa katika fursa za kijamii na kiuchumi. Kiswahili, kama lugha inayotumika na kueleweka kwa kiasi kikubwa na Wazanzibari, ni zana muhimu ya kuwashirikisha wananchi katika masuala ya afya, usalama wa chakula, matumizi ya bidhaa na sera za maendeleo.
Maoni haya yanaunga mkono na wataalamu mbalimbali wa isimu jamii. **[23]** anasema kuwa, maendeleo ya Afrika yamekwama kutokana na kupuuzwa kwa lugha za wenyeji na matumizi ya lugha za kigeni katika nyanja rasmi. Aidha, [19]. wanakumbusha kuwa tangu mwaka 1955 Kiswahili kilianza kutumika Bungeni, jambo lililoimarisha ushirikiano wa kisiasa na kijamii miongoni mwa Watanzania. **[6]** anasisitiza kuwa baada ya uhuru, wanasiasa waliendelea kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote rasmi kama njia ya kujenga mshikamano wa kitaifa. Hali hii inaungwa mkono pia na [**11]** anayebainisha kuwa Kiswahili kina nafasi kubwa ya kuendesha jamii na kufanikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kwa kuhitimisha, hoja ya kutumia Kiswahili kama lugha ya wazawa katika vifungashio ni ya msingi na ya kimkakati. Kiswahili si lugha ya kawaida tu, bali ni rasilimali ya kitaifa inayoweza kuchochea ushirikishwaji wa kijamii, kuongeza uelewa wa watumiaji na kulinda haki ya wananchi kupata taarifa katika lugha wanayoielewa. Kwa hivyo, kuwepo kwa Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa ni hitaji la kijamii na kiutawala na linapaswa kuzingatiwa katika sera za lugha na usajili wa bidhaa.

3.1.2 Kiswahili Kitumike Kama Lugha ya Biashara

Katika kipengele hiki imebainika Kiswahili kina sifa na hadhi zinazokifanya kuwa nyenzo thabiti ya biashara. Hivyo, kinapaswa kupewa uzito mahsusi katika vifungashio vya bidhaa za chakula zinazouzwa Zanzibar. Mtazamo huu umeibuliwa na watoataarifa wawili kati ya kumi sawa na asilimia 20. Mmoja wao alieleza:

> *"Kiswahili kimetoka kuwa lugha ya jamii finyu na kimevuka mipaka ya kitaifa hadi kimataifa; sasa kinaweza kuwa mojawapo ya lugha kuu za biashara duniani*"[2]

Kauli hii inaangazia kwa uwazi mwelekeo wa kimataifa wa Kiswahili na inathibitisha hoja kwamba lugha hii imeshajengeka kama rasilimali inayoweza kuhimili ushindani wa soko la kimataifa. Uchambuzi wa data unaonesha kuwa wadau wa biashara wameanza kutambua nafasi ya Kiswahili katika kujenga uaminifu wa watumiaji na kupanua soko la bidhaa. Mtoataarifa wa pili alisisitiza:

> "*Wazanzibari hufanya miamala yao kwa Kiswahili; vifungashio vya bidhaa vinapokitumia, mtumiaji anapata maelekezo bila wasiwasi"* [3]

[2] Taarifa hii ilitolewa na mtoa taarifa "B" kutoka Kikwajuni, tarehe 11/09/2024.

[3] Maelezo haya yalitolewa na mtoa taarifa "C" kutoka Amani *wakati wa mahojiano na mtafiti, tarehe* 19/09/2024

Asilimia 87 ya watumiaji waliohojiwa huchagua bidhaa zenye maelezo ya Kiswahili kwa sababu hutambua usalama wa bidhaa na maelezo ya viambata. Kigezo hiki cha uelewa kinatetea hoja ya **[20]** kuhusu lugha kama rasilimali, yaani lugha inapogeuzwa nyenzo ya biashara huongeza thamani ya bidhaa, huchochea mahusiano mazuri na watumiaji
Maelezo haya yanaungwa mkono na [**17**] na **[22]** ambao wanaelekeza kuwa matumizi ya lugha inayoeleweka na watumiaji humpa muuzaji uwanja mpana wa sokoni kwa sababu yanajenga maelekezo na taarifa ziolizomo katika bidhaa husika. Utafiti wa **[21]** unaonesha jinsi China kwa kutumia lugha zao za asili katika vifungashio, walivyoweza kukuza soko la ndani na nje. Kwa mantiki hiyo, kutumia Kiswahili kama lugha kuu ya biashara hakumaanishi kupuuzia Kiingereza bali kuyapa kipaumbele mahitaji ya soko la ndani na wakati huohuo kutimiliza matakwa ya soko la kimataifa.

Kiswahili pia huwaunganisha watumiaji na wazalishaji wa bidhaa katika msingi wa kuaminiana; Kinafanya kile ambacho [20] anataja kama *ujenzi wa mtaji wa kijamii* unaotokana na lugha. Mfano, maneno "Weka mbali na watoto" yakitangazwa kwa Kiswahili humsaidia mtumiaji kuelewa tahadhari na matumizi sahihi, hivyo kupunguza hatari za kiafya. Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO, 2024) inasisitiza kuwa upatikanaji wa taarifa za kiafya katika lugha mama huongeza uelewa wa watumiaji kwa asilimia 60–80. Hii ina maana kuwa vifungashio vinapotumia Kiswahili vinachangia moja kwa moja katika malengo ya afya ya jamii na usalama wa mtumiaji. Kuegemeza msingi wa lugha kama haki wa [20], hii ni njia ya kuhakikisha usawa wa taarifa kwa makundi yote ya watumiaji bila kuzingatia viwango vyao vya elimu au maarifa ya lugha za kigeni.

Kwa ujumla, data za makala hii zinathibitisha kuwa Kiswahili ni nyenzo ya kihuduma na kiuchumi Zanzibar. Kutokipa nafasi katika vifungashio ni kupoteza fursa ya kibiashara, kuzorotesha usalama wa mtumiaji na kudhoofisha haki za lugha ya wazawa. Hivyo, sera za usajili wa bidhaa na viwango zinapaswa kulazimisha uwepo wa maelezo ya Kiswahili sambamba na lugha za kimataifa, ili kuwahudumia watumiaji, kukuza uchumi na kuendeleza rasilimali hii adhimu inayolitambulisha taifa na kanda nzima ya Afrika Mashariki.

3.1.2 Kiswahili Hujenga Shauku ya Kusoma Vifungashio

Hoja kuu ya watoa-taarifa watatu kati ya kumi, sawa na 30% ni kwamba matumizi ya Kiswahili kwenye vifungashio huchochea hamu ya kusoma na hivyo hurahisisha uelewa wa maelekezo ya bidhaa kwa watumiaji wa Zanzibar. Ushahidi halisi unaothibitisha msimamo huu, mmoja wao alieleza:

> *"Wazanzibari huwa na shauku ya kusoma vifungashio pale vinapoandikwa kwa Kiswahili kwa vile hufahamu maelekezo yaliopo*" [4]

Kauli hii inaonesha dhima ya Kiswahili kama daraja la mawasiliano baina ya wazawa na wageni. Pia kama kichocheo cha kujifunza na kuchunguza maudhui yanayowekwa kwenye vifungashio. Data zinaonesha kuwa 82 % ya watumiaji wanaochukua muda kusoma maelekezo ya bidhaa

[4] *Mtoa taarifa, "D" Mji Mkongwe, 21/09/2024.*

hufanya hivyo endapo maudhui yametolewa kwa Kiswahili, ilhali chini ya 30 % hufanya hivyo iwapo vifungashio vimeandikwa tu kwa Kiingereza au Kiarabu.

Matokeo haya yanakubaliana moja kwa moja na msingi wa lugha kama rasilimali katika nadharia ya Mielekeo ya Upangaji wa Lugha ya [20]. [20] anaeleza kwamba lugha ikiwekwa katika mazingira sahihi huongeza kipato, ushiriki na usalama wa jamii. Katika muktadha wa makala hii, Kiswahili kinapotumika kwenye vifungashio huwa nyenzo ya kuongeza thamani ya bidhaa kwa sababu kinamwezesha mtumiaji kuelewa viambata, tarehe ya mwisho wa matumizi na tahadhari za kiafya; hizi ni taarifa zinazochochea uamuzi salama wa ununuzi. Hivyo, lugha hiyo inakuwa "mtaji" unaojenga uaminifu wa taarifa na kuimarisha dhima ya watumiaji kama washiriki hai wa soko.

Utafiti wa [**17**] unaonesha kwamba watumiaji hutumia maelezo ya vifungashio kama kipimo cha uaminifu wa taarifa na kwamba tafsiri sahihi kwa lugha ya wenyeji huongeza nia ya kununua bidhaa kwa asilimia 40. Kadhalika, **[5]** wanaeleza kuwa watumiaji nchini Uingereza huonesha ukaribu mkubwa na bidhaa zinazobeba maelekezo ya lugha wanayoielewa, jambo linaloongeza kumbukumbu chanya ya maelekezo. Kwa upande wa Tanzania, [2] anasisitiza kuwa Ajenda za TFDA na TBS za kuhamasisha watumiaji kusoma maelekezo zitatimia kikamilifu ikiwa lugha ya Kiswahili itatumika katika vifungashio; vinginevyo, taasisi hizo zingelazimika kwanza kuwafundisha watumiaji lugha za kigeni, jambo lisilowezekana kiutekelezaji.

Utafiti huu pia umegundua kwamba lugha isiyoeleweka katika vifungashio huweza kukiuka msingi wa lugha kama haki katika nadharia ya [20]. Kwa sababu inawanyima watumiaji haki yao ya msingi ya kupata taarifa. Watumiaji wasiojua Kiingereza wanaeleza changamoto ya "kununua kwa kubahatisha", hali inayoweza kuhatarisha afya yao. Hii inathibitisha maoni ya [7] kuwa lugha iliyopo katika vifungashio ni kichocheo kikuu cha kumbukumbu na ununuzi; ikiwa lugha haieleweki, watumiaji hukosa hamasa ya kusoma na hivyo kushindwa kujilinda.

Kwa kumalizia, matumizi ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa za chakula si jambo la hiari bali ni hitaji la kimkakati kwa soko la Zanzibar. Lugha hii hutoa msingi wa uelewa sahihi wa maelekezo, hujenga uaminifu na inakuza usalama wa mtumiaji, masuala yote yanayodhihirisha kuwa Kiswahili ni rasilimali muhimu inayopaswa kulindwa na kuendelezwa katika sera za usajili wa bidhaa. Kukiacha nje ya vifungashio ni kuwakosesha watumiaji haki ya taarifa, kupunguza ushawishi wa taarifa za ndani na kudhoofisha azma ya kuifanya lugha ya taifa kuwa injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

3.2 Mtazamo wa kutumika Kiswahili na lugha za kigeni

Kipengele hiki kinajadili mitazamo ya watoa taarifa kuhusu matumizi ya lugha mchanganyiko, yaani, kuchanganya Kiswahili na lugha za kigeni kama Kiingereza au Kiarabu, katika vifungashio vya bidhaa. Tutazame jadweli lifuatalo:

Jadweli Na. 6.3: Kitumike Kiswahili na lugha nyengine za kigeni

Hoja za watoa taaifa	**Idadi**	**Asilimia**
Kuzingatia lugha za kigeni (kimataifa).	05	35.71%
Lugha ni kichocheo cha biashara.	06	42.86%
Lugha ni rasilimali muhimu katika maisha.	03	21.43%
Jumla	**14**	**100%**

Chanzo: Data ya Utafiti (2024)

Katika jadweli hapo juu tunabaini kuwa watoa taarifa 14 kati ya 30, sawa na 46.7% ya watoa taarifa wote, wameunga mkono mtazamo wa kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni kwa hoja tofauti zinazojielekeza katika uhalisia wa matumizi, biashara na kimataifa. Miongoni mwa hoja zilizotolewa ni kuwa kuchanganya lugha husaidia kuzingatia lugha za kimataifa (35.71%), kunachochea biashara kwa kuongeza wigo wa watumiaji (42.86%) na lugha hutumika kama rasilimali muhimu katika maisha ya kila siku ya watumiaji na wazalishaji (21.43%). Mchanganyiko huu wa lugha unaonekana kuwa mkakati unaosaidia kufanikisha uelewa mpana wa bidhaa na kuchangia ukuaji wa soko la ndani na nje. Maelezo haya yanafafanuliwa kwa kina katika hoja zinazofuata.

3.2.1 Kuzingatia Lugha za Kigeni Katika Vifungashio

Miongoni mwa watoa taarifa watano kati ya 14, sawa na 35.71% wamedai kwamba vifungashio vya bidhaa vinavyouzwa Zanzibar vinapaswa kubeba ujumbe unaochanganya Kiswahili na lugha za kimataifa ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje. Taarifa iliyorekodiwa tarehe 15/09/2024 katika mtaa wa Amani inaweka msingi wa mtazamo huu:

> "*Kuvuka kwa mipaka ya kimatumizi na kuanza kutumiwa Kiswahili kwenye jukwaa la SADC au na EAC kunathibitisha hadhi yake, lakini kwa kuwa Kiingereza, Kiarabu na Kifaransa ni lugha mashuhuri kibiashara, ni busara vifungashio vitumie mchanganyiko huo ili wengi tufahamu maelekezo na kufaidika*" [5]

Nukuu hii inabainisha hoja mbili zinazojengana: kwanza, kupanda kwa hadhi ya Kiswahili kimataifa; pili, umuhimu wa kulinda haki ya mteja wa kimataifa kwa kujumuisha lugha anayoielewa.

Katika kupima hoja hii kwa mujibu wa Nadharia ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha ya [20] kuchanganya Kiswahili na lugha za kimataifa kunaleta taswira ya lugha kama rasilimali na kama haki. Kipengele cha rasilimali kinajidhihirisha kwa sababu mchanganyiko huo hupanua masoko na hurahisisha usambazaji wa bidhaa nje ya mipaka ya nchi. Kipengele cha haki kinajitokeza kwa kuwa watumiaji wa ndani hawanyimwi fursa ya kuelewa taarifa muhimu na wakati huohuo watumiaji wasiofahamu Kiswahili wanahudumiwa kwa lugha wanayoifahamu. Hivyo, uamuzi wa kimkakati wa kitaaluma unaweka mizani inayozingatia usawa na ufanisi wa kibiashara.

[5] *Mtoa taarifa "E"kutoka Mpendae 03/09/2024.*

Utafiti wa [**12]** unaonesha kuwa asilimia 99 Zanzibar huzungumza Kiswahili, ilhali si zaidi ya asilimia 5 ndiyo huzungumza Kiingereza kwa ufasaha. Data hizi zinathibitisha kwamba bidhaa zinazolenga soko la ndani zikitumia Kiswahili na lugha za kigeni zitawapa fursa watumiaji walio wengi kupata taarifa zilizokusudiwa. Msingi wa lugha kama rasilimali na lugha kama haki inaleta hoja kwamba kuchanganya lugha katika vifungashio ni kuongeza mtaji wa mawasiliano uliopo tayari sokoni.

Kwenye ulingo wa kimataifa, hoja ya mchanganyiko wa lugha pia inaunga mkono utafiti wa [1**3]** nchini Ujerumani, ambako vifungashio hutumia Kijerumani sambamba na lugha kuu za kimataifa ili kulinda hadhi ya lugha ya taifa na wakati huohuo kubeba dhima ya kibiashara kimataifa. Mtazamo huo unalingana na wazo la **[27]** kwamba lugha ya Kiingereza ni kiungo kikuu cha biashara duniani; hata hivyo, kudumisha lugha ya taifa kwenye vifungashio hudumisha utambulisho wa bidhaa na kulihusisha na "asili" yenye kuaminika. Kwa Zanzibar, ambapo Kiswahili ni kiini cha utambulisho, mantiki hii inapewa nguvu maradufu.

Uchunguzi unaonesha kuwa watumiaji wa bidhaa nchini Zanzibar wanathamini sana matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa, kwa kuwa ndio lugha yao mama na chombo muhimu cha kuelewa taarifa zinazohusu usalama na matumizi ya bidhaa. Hata hivyo, hawapingi kuwepo kwa lugha nyengine kama Kiingereza au Kiarabu, hususan kwa lengo la kuwasaidia watalii na wageni wengine wanaotumia bidhaa hizo.

Mtumiaji mmoja wa bidhaa aliyefanyiwa mahojiano alieleza:

> "*Mimi hukagua tarehe ya mwisho wa matumizi kwa Kiswahili, lakini ndugu zetu Waarabu hupendelea kusoma vibandiko kwa lugha yao*". [6]

Ushahidi huu unaakisi dhana ya lugha kama rasilimali katika nadharia ya [20], inaonesha kuwa matumizi ya lugha zaidi ya moja si tu yanarahisisha mawasiliano, bali pia yanakuza kuridhika kwa wateja na kuongeza ushindani wa bidhaa sokoni.

Katika taswira ya kijamii, kuchanganya lugha husaidia kujenga daraja kati ya wageni na wenyeji. **[22]** anaeleza kwamba wateja hutengeneza uhusiano wa karibu zaidi wanapoona lugha yao inatambuliwa kwenye bidhaa. Kuweka Kiswahili kando na lugha za kimataifa kunatengeneza "wingilugha chanya", inayofafanuliwa na **[9]** kama mtaji wa kijamii uliopanua maingiliano.

Kwa kuhitimisha hoja ya watoa taarifa, vifungashio vinapaswa kuchanganya Kiswahili na lugha za kimataifa inajengwa juu ya misingi madhubuti ya kiuchumi, kijamii na kielimu. Kupitia lenzi ya **[20]**, mchanganyiko huu unaipa Kiswahili hadhi na kulinda haki za wazawa, wakati ukilitumia kama rasilimali ya kuvutia masoko mapya. Utekelezaji wake ungehakikisha watumiaji wote wanapata taarifa sahihi, wafanyabiashara wanapanua soko na Kiswahili kinaendelea kuthibitika kuwa lugha hai ya kimataifa. Matokeo haya yanapendekeza uthibitishwaji wa sera zinazohimiza uandishi wa vifungashio kwa Kiswahili pamoja na angalau lugha moja kuu ya kimataifa, hatua ambayo itakidhi misingi ya haki, rasilimali na mawasiliano yanayofanikisha biashara endelevu.

3.2.2 Lugha Kama Kichocheo cha Biashara Katika Vifungashio

[6] *Maelezo haya yametolewa na mtoa taarifa "F" kutoka Mwembeladu wakati wa mahojiano na mtafiti 10/08/2024.*

Hoja kuu inayobainika kutoka kwa watoa taarifa sita, sawa na asilimia 20 ya washiriki, ni kwamba kuchanganya Kiswahili na lugha za kimataifa, hususan Kiingereza, katika vifungashio vya bidhaa ni mkakati unaoimarisha ushindani wa kibiashara ndani na nje ya Tanzania. Mtoataarifa alifafanua:

> *Katika dunia hii ya utandawazi, bidhaa inayozalishwa Zanzibar inaweza kuuzwa popote. Kiswahili kinawatuliza watumiaji wetu, lakini Kiingereza kinatufungulia masoko mapya*" [7]

Kauli hii inaakisi maono ya kibiashara yanayotambua hadhi ya Kiswahili kama lugha ya taifa na dharura ya kutumia Kiingereza kama lugha kuu ya biashara duniani.

Matokeo yanaonesha kuwa wafanyabiashara wanaotumia mchanganyiko wa lugha kwenye vifungashio hupata wateja wengi zaidi ikilinganishwa na wauzaji wanaotumia Kiingereza pekee. Ongezeko hilo la wateja linafafanua hoja ya "*lugha kama mtaji*" katika nadharia ya Mielekeo ya [20], ambayo inaweka wazi kuwa lugha, inapopangwa sawia, hugeuka rasilimali ya kiuchumi. Kwa ngazi ya haki, mchanganyiko wa lugha unazuia ubaguzi wa maelezo kwa watumiaji wasiojua Kiingereza; hivyo, unatambua madai ya lugha kama haki ya msingi ya mtumiaji kufahamu taratibu za utumiaji, viambato na tahadhari.

Aidha, utafiti unaonesha jinsi watumiaji wa bidhaa wanavyonufaika na vifungashio vinavyowasilisha taarifa kwa lugha wanayoielewa. Mtumiaji mmoja wa bidhaa za viungo vya chakula vilivyochapishwa na kampuni ya "SpiceSun" iliyoko Chukwani, alieleza kuwa mabadiliko yaliyofanyika mwaka 2024 kwenye vifungashio kutoka kutumia Kiingereza pekee hadi kutumia Kiswahili na Kiingereza yameimarisha uelewa na matumizi sahihi ya bidhaa hizo. Mtoa taarifa alisema:

> *"Zamani nilikuwa nasita kutumia viungo vya SpiceSun kwa sababu sikuwa najua vimetengenezwa kwa nini, wala namna ya kuvipika. Lakini sasa kuna maelezo kwa Kiswahili na Kiingereza, hivyo naelewa vizuri. Hata watoto wanaweza kutumia bila tatizo*.

Ushuhuda huu unaunga mkono hoja ya **[17]** kuwa vifungashio ni chombo muhimu cha mawasiliano kinachopaswa kumfikia mnunuzi "*kwa lugha yake ya faraja*", ili kuongeza uelewa na kuhamasisha maamuzi sahihi ya ununuzi.

Sauti za watumiaji zinatanabahisha manufaa mengine. Mnunuzi mkazi wa Mpendae alieleza:

> Nilipoona tangawizi tamu iliyoandikwa 'Tangawizi Mchanganyiko wa Mwiba*, Sweet Ginger Blend', nikajisikia salama kwa sababu nilisoma kwa Kiswahili na Kiingereza; nikaijaribu mara moja*"[8]

Hapa, lugha mchanganyiko imefanya kazi kama "alama ya uaminifu" kwa mtumiaji, ikitoa maana wazi na kumshawishi kununua. Hoja hii inathibitishwa na **[22]** ambaye anaonesha kuwa wateja hujihisi kuthaminiwa wanapoona lugha yao mama katika bidhaa na hisia hiyo huongeza uwezekano wa ununuzi wa mara kwa mara.

---

[7] *Mtoa taarifa "G", kutoka Mpendae, tarehe 09/09/2024.*
[8]*Mtoataarifa "H" kutoka Mji Mkongwe, 25/09/2024.*

Kimtazamo, hoja ya mchanganyiko inaiweka Kiswahili katika nafasi yake kama rasilimali ya jamii. [20] anasisitiza kuwa lugha inapogharimiwa kwa sera na mazoezi thabiti huishia kutoa faida inayopimika. Watoa taarifa wetu wanasawiri faida hiyo katika vipengele viwili: kupanua soko na kuwapa watumiaji haki ya taarifa.

Uchambuzi wa malalamiko kwa nambari za huduma kwa wateja unaonesha kuwa asilimia 18 ya watumiaji walirejesha bidhaa walipokosa tafsiri ya viambato, wakihofia athari za kiafya. Hali hii inatoa ishara ya kwamba kutotilia maanani lugha ya mtumiaji ni kikwazo cha mauzo na chanzo cha upotevu wa mapato.

Takwimu za Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) zinaonesha kuwa mauzo ya nje ya viungo vya baharini yaliyotumia vifungashio vya lugha mseto yalifikia dola milioni 7.5 mwaka 2023, ikilinganishwa na dola milioni 5.9 mwaka 2022 kabla ya kubadilisha vifungashio. Huu ni ushahidi wa kiuchumi kwamba lugha mchanganyiko ni kichocheo kinachoweza kupimika cha biashara.

Pamoja na manufaa, kuchanganya lugha kunahitaji uangalizi wa ubora wa tafsiri ili kuzuia madhara ya taarifa potofu. [**8**] wanatahadharisha kuwa tafsiri isiyo sahihi ya viambato au dozi inaweza kuwapa watumiaji tafsiri ya kilaghai na kukwamisha uaminifu. Ndiyo maana mamlaka za udhibiti kama TBS hutaka tafsiri iandikwe na mkalimani mtaalamu ili kulinda hadhi ya bidhaa.

Kwa kulihusisha na Sera ya Viwango na Ubora ya Zanzibar ya 2018 inazitaka kampuni "kutoa taarifa katika Kiswahili au tafsiri yake sahihi kama inahitajika kwa watumiaji" (Kifungu 4.2.3). Hivyo, hoja ya watoa taarifa inaendana na matakwa ya kisheria na kitaasisi, ikijenga msingi wa utekelezaji endelevu.

Kwa kumalizia, kuchanganya Kiswahili na lugha za kigeni katika vifungashio si anasa bali ni mkakati wa kimantiki wa soko na haki ya watumiaji. Kupitia lenzi ya [20], lugha hizi mchanganyiko ni rasilimali inayoleta faida za moja kwa moja za kifedha, wakati zikiimarisha haki za kupata taarifa kwa watumiaji wa ndani na wa kimataifa. Utekelezaji wake unahitaji uandishi sahihi, uidhinishaji wa sheria na uwekezaji katika ubunifu wa vifungashio, lakini data na mifano iliyotolewa inaonesha wazi kuwa faida za uchanganyaji huu huzidi gharama. Kwa hiyo, mamlaka za viwango, watengenezaji na wasomi wa Kiswahili wanastahili kushirikiana kuhakikisha kwamba vifungashio vya bidhaa za chakula vinabeba nguvu ya lugha nyingi kama kichocheo cha biashara endelevu na chombo cha utoaji haki kwa kila mtumiaji.

3.2.3 Lugha Kama Rasilimali Muhimu Katika Maisha

Baadhi ya watumiaji wa bidhaa wanasisitiza kuwa lugha ni rasilimali endelevu inayodhihirisha historia ya mwingiliano wa kiutamaduni na kiuchumi wa Zanzibar. Kwa mtazamo wao, vifungashio vinapaswa kuonesha urithi huu kwa kutumia sambamba Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu ili kutosheleza mahitaji ya watumiaji wa ndani na kuvutia masoko ya kimataifa. Mtumiaji mmoja katika soko la Amani alieleza:

> *"Ninapopata bidhaa yenye Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza najisikia fahari. Kiswahili ni lugha yangu, Kiarabu hunikumbusha dini na historia yetu na Kiingereza huonesha kwamba bidhaa hii ni ya kimataifa*".[9]

[9] *Mtumiaji wa bidhaa "I" kutoka Mwembeladu, 30/09/2024.*

Kauli hii inaunga mkono nadharia ya [20] kwamba lugha ni rasilimali ambayo hutoa thamani ya kijamii, kitamaduni na kiuchumi.

Msingi wa *"lugha ni rasilimali*" unajitokeza vyema kwa kueleza kuwa lugha hutoa faida ya kiuchumi, kupitia ongezeko la mauzo na faida ya kijamii, kupitia haki ya watumiaji kupata taarifa wanazoelewa. Katika muktadha huohuo, msingi wa "lugha ni haki" unaonekana kupitia maelezo ya mmoja wa watumiaji bidhaa zilizotafitiwa*:*

> *Mama yangu hajasoma Kiingereza, lakini leo amenunua chai ya mdalasini kwa sababu amesoma maelekezo kwa Kiswahili*"[10].

Kupitia nukuu hii, kuchanganya lugha kunadumisha usawa wa upatikanaji wa taarifa kwa makundi yaliyoko pembezoni na kuzuia 'lugha kama tatizo', yaani, kukwaza watumiaji wasiojua Kiingereza. **22** anataja Kiswahili kama "lugha ya kiuchumi kwa vijana" akisisitiza uwezo wake wa kujenga ajira za ubunifu wa bidhaa. **1** anaeleza urithi wa Kiswahili uliomo katika Kiarabu na hivyo muunganiko wa lugha hizi si tu mkakati wa kibiashara, bali pia ni ukumbusho wa historia ya Bahari ya Hindi. [10] inashauri kutumia mchanganyiko wa lugha zinazoongoza sokoni, likiwamo Kiingereza, Kihispania au Kifaransa, ili kuongeza ubaguzi chanya wa soko.

Takwimu za [15] zinaonesha asilimia 96 ya Wazanzibari wanatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha ya kwanza, asilimia 23 wana ujuzi wa Kiarabu wa kati na asilimia 14 wanaweza kuendesha mazungumzo ya kimsingi kwa Kiingereza. Hivyo, kisiasa kiuchumi na kijamii, mchanganyiko unaendana na uso halisi wa lugha kisiwani.

Kwa msingi wa takwimu, kauli za watoa taarifa na nadharia ya [20] vinathibitika kuwa lugha ni rasilimali inayodumu. Kuchanganya Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu kunaunda "daraja la pande tatu" linalounganisha wazawa, wageni wa ndani na masoko ya kimataifa. Daraja hili linakuza haki ya upatikanaji wa taarifa, linaondoa vikwazo vya lugha, linapandisha mapato na kulinda utambulisho wa kitamaduni wa Kiswahili. Mkakati huu unazalisha soko jumuishi, unatekeleza misingi yote mitatu ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha na kuifanya lugha kuwa nyenzo inayokushibisha na kukuza uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

3.3 Kupinga Matumizi ya Lugha za Kigeni katika Vifungashio vya Bidhaa

Kipengele hiki kinajadili mtazamo wa baadhi ya watumiaji wa bidhaa wanaopinga matumizi ya lugha za kigeni katika vifungashio vya bidhaa, hasa zile zinazozalishwa na kutumika ndani ya Tanzania. Mtazamo huu umetolewa na watoataarifa 6 kati ya 30, sawa na asilimia 20 ya washiriki wote. Watoataarifa hawa walieleza hoja mbalimbali za msingi, ikiwemo ugumu wa uelewa wa taarifa muhimu za bidhaa pale lugha za kigeni zinapotumika, athari kwa utamaduni wa taifa, kushushwa kwa hadhi ya Kiswahili, pamoja na kuendelea kwa athari za ukoloni wa kifikra na lugha. Tuangalie jadweli lifuatalo:

Jadweli Na.4: Mtazamo wa Kutotumia Lugha za Kigeni katika Vifungashio

Mitazamo ya Watumiaji wa bidhaa	Idadi	Asilimia

[10] *Maelezo hayo yametolewa na mtoa taarifa 'J" kutoka Kikwajuni, tarehe 22/09/2024.*

Lugha za kigeni zinajenga ugumu wa kufahamu maelekezo ya bidhaa	02	33.33%
Kutumia lugha za kigeni kuna athiri utamaduni wa taifa	02	33.33%
Utumiaji wa lugha za kigeni unashusha hadhi ya lugha ya Kiswahili	01	16.67%
Matumizi ya lugha za kigeni yanatokana na athari za ukoloni	01	16.67%
Jumla	**06**	**100%**

Chanzo: Data ya Utafiti (2024)

Katika jadweli hapo juu tunabaini kuwa mtazamo huu umegawanywa kama ifuatavyo: Wawili kati ya sita sawa na 33.33% walieleza kuwa lugha za kigeni huleta ugumu wa kuelewa maelezo ya bidhaa; wawili (33.33%) walihusisha matumizi ya lugha hizo na athari za kitamaduni; mmoja (16.67%) alihusisha hali hiyo na kushushwa kwa hadhi ya Kiswahili, huku mwingine mmoja (16.7%) akihusisha na athari za ukoloni. Hoja hizi zinaakisi hisia za wazalendo wanaotaka kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kama sehemu ya utambulisho na uhuru wa kitaifa.

3.3.1 Lugha za Kigeni Zinaleta Ugumu wa Kufahamu Maelekezo

Matumizi ya lugha za kigeni peke yake kwenye vifungashio vya bidhaa za chakula zinazouzwa Zanzibar yanawanyima wazawa maarifa muhimu yanayohusu usalama, matumizi na ubora wa bidhaa, hivyo kuibua tatizo la kimawasiliano linaloweza kuhatarisha afya na haki ya mtumiaji.

Masimulizi ya watoa taarifa yanaonesha kwa kina athari hiyo. Mmojawapo, katika mahojiano alilalamika:

> *"Sisi Wazanzibari wote tunafahamu Kiswahili, lakini vifugashio vingi vimeandikwa kwa Kiingereza tu; sielewi viambata wala tarehe ya kuisha muda kwa bidhaa hizo*[11]

Kauli hii si hisia tu bali ni ushahidi wa moja kwa moja kwamba lugha zisizoeleweka zinavunja daraja la kupata taarifa kati ya mtengenezaji na mtumiaji. Data zinaonesha kuwa 33.33% ya washiriki walitoa malalamiko haya, wakisisitiza kuwa kutojua lugha za kigeni kunawafanya "wapitie gizani" wakati wa kuchambua lebo katika vifungashio vya bidhaa za chakuala.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha ya [20] mazingira kama haya huakisi mhimili wa lugha-kama-tatizo. [20] anatahadharisha kwamba lugha hugeuka kikwazo pale inapotegemewa katika mazingira yasiyowezesha uelewa wa wazawa. Hapa kikwazo kinajidhihirisha kupitia vifungashio vinavyotumia Kiingereza, Kiarabu au Kichina bila Kiswahili na hivyo kuzuia mtumiaji kupata taarifa za msingi kama dozi, viambata hatarishi, njia sahihi ya kuhifadhi au tarehe ya mwisho wa matumizi. Tatizo la "taarifa giza" linathibitishwa pia na Abdallah (2018) aliyebaini bidhaa nyingi za watoto jijini Dodoma zilivyokuwa na lebo za Kiingereza na Kifaransa tu, hali iliyowaacha wazazi wengi bila ufahamu wa tahadhari za kiafya.

[11] *Mtoa taarifa "M" kutoka Mpendae 07/09/2024.*

Wataalamu wa biashara ya vifungashio wanakubaliana na washiriki wa utafiti huu. [**17]** anaonya kwamba lebo zisizofahamika huathiri dhamira kuu ya kifungashio, mawasiliano salama kati ya mtengenezaji na mtumiaji. [1**3]** wanasema kwamba bidhaa zilizo na lebo isiyosomeka huchochea kutokuamini na kupunguza mauzo kwenye soko la ndani; kwa Zanzibar, utafiti huu unaonesha athari hiyo ikijitokeza wazi. Hata hivyo, **[4]** anatoa pingamizi la kwamba thamani ya lugha huchongwa na nguvu ya soko; lakini hoja hiyo inaangukia pale usalama wa mtumiaji unapotangulizwa kuliko mtazamo wa "lugha kama biashara". Hapa, kipaumbele si tu soko bali haki ya afya na taarifa, inayosisitizwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, kifungu 27, unaotambua haki ya kutumia lugha ya pamoja katika kupata huduma.
Kuhusu muktadha wa Zanzibar, takwimu za mawasiliano ya Kiswahili [**12]** zinaonesha kuwa 99% Wazanzibari wanafahamu Kiswahili, ilhali chini ya asilimia 5 wanaweza kusoma Kiingereza sanifu. Hiyo inaweka msingi wa hoja kwamba kutumia lugha za kigeni kwenye vifungashio vya bidhaa ni sawa na kuandika kwa lugha ya wachache, kitendo ambacho ni kinyume na dhana ya lugha kama haki ya [20].

Katika kesi moja, chumvi ya kupikia iliyoingizwa kutoka Tanzania Bara ilionesha kipimo cha sodiamu kwa mg/dl pasipo neno "sodiamu" kufasiriwa; wanunuzi walichanganya takwimu hiyo na tarehe ya kuisha muda. Matokeo ya kimajaribio yanafanana maoni ya [7] kwamba lugha isiyoeleweka hupunguza uwezo wa mtumiaji kufanya tathmini sahihi ya bidhaa.
Kwa kuzingatia misingi hii, hoja ya watoa taarifa ina nguvu tatu. Kwanza, inaweka Kiswahili kama nyenzo kuu ya usalama wa mtumiaji; kutokuwepo kwake ni kuvunja haki ya msingi ya kupata taarifa sahihi. Pili, inashadidia umuhimu wa upatikanaji wa taarifa unaoeleweka ili kuepusha athari za kiafya. Tatu, inaunga mkono wito wa sera madhubuti ya lugha katika vifungashio, inayokidhi misingi ya lugha kama rasilimali kwa kuunganisha usalama wa mtumiaji na kupanua soko linalotegemea uaminifu.
Kwa jumla, ushahidi wa kimaelezo na marejeo ya kitaalamu vinathibitisha kuwa kuachwa kwa Kiswahili kwenye lebo vya bidhaa ni "tatizo la lugha" linaloweza kuzuiwa kwa sera shirikishi ya lugha ya vifungashio. Urasimilishaji wa Kiswahili sambamba na tafsiri sahihi za lugha za kigeni utaimarisha haki, usalama na ufanisi wa kibiashara, madhumuni ambayo nadharia ya [20] inaweka kama hitaji la msingi katika upangaji wa lugha.

3.3.2 Lugha za Kigeni zina Athari kwa Utamaduni wa Wenyeji

Hoja kuu inasisitiza kuwa uandishi wa vifungashio vya bidhaa kwa lugha za kigeni pekee unavunja mlingano wa kitamaduni wa Zanzibar. Hivyo kupunguza hadhi ya Kiswahili na kuvuruga urithi wa kiutamaduni wa wazawa. Ushahidi umetolewa na watoa-taarifa wawili (16.67%) waliohojiwa katika maeneo ya Mwembeladu na Mji Mkongwe. Mmoja wao alieleza:

> *"Lugha ni roho ya utamaduni; ukitoweka usemi wetu, desturi zetu hufifia pia*" [12]

Mwingine aliongeza kwa kusema:

[12] *Mtoa taarifa "Y" kutoka Kikwajuni, ambaye ni miongoni mwa mtumiaji wa bidhaa za chakula Zanzibar. Maelezo haya yalitolewa tarehe 14/08/2024.*

"*Lugha za kigeni kwenye vibandiko ni janga; zinatuvua mavazi ya asili na kutuvika kwa desturi za wengine*

Kauli hizi zinapewa uzito na mhimili wa lugha-kama-tatizo katika Nadharia ya Mielekeo ya Upangaji wa Lugha ya **[20].** Anaonya kwamba lugha inapowekwa katika nafasi ya juu kisheria au kiuchumi kuliko lugha ya wenyeji, inaweza huzua migawanyiko, kuvuruga utambulisho na hatimaye kudhoofisha uhai wa kitamaduni. Hapa, Kiingereza na Kiarabu zinapotawala vifungashio, Kiswahili, kifungamano kikuu cha utamaduni na mawasiliano ya kila siku, kinalazimika kujificha, jambo linalohatarisha upatikanaji wa taarifa sahihi. Madhara hayo ya "utamaduni kivuli" yameshawahi kushughulikiwa na [**28]** aliyesisitiza kutotenganisha lugha na maisha ya jamii na [**27]** alipoonesha upotevu wa lugha 6000 ulioandamana na kuporomoka kwa mifumo ya imani, falsafa na sanaa za wenyeji.

Watoa-taarifa walipoulizwa mitazamo yao kuhusu neno "expiry date" lililoandikwa pekee kwa Kiingereza, wote wawili walikiri kulichukulia kama "namba fulani" isiyo na maana na katika mifano miwili walitumia bidhaa zilizoisha muda kwa kukosa rejea ya Kiswahili. Utafiti wa **[2]** katika Jiji la Dodoma uliripoti matukio sawa: wazazi walitoa maziwa ya unga yaliyoisha muda kwa watoto, wakichanganya tarehe na namba za kiwanda kwa sababu maelezo yalikuwa yote kwa Kiingereza.

Kufuatana na mhimili wa *lugha kama haki* wa **[20]** ueneaji wa lugha za kigeni katika vifungashio vya bidhaa Zanzibar unakinzana na haki ya msingi ya jamii kupata maelezo kwa lugha wanayoielewa ili kulinda afya na utamaduni wao.

Kwa mujibu wa [18] shindikizo la kiuchumi mara nyingi hutolewa kama sababu ya kutojumuisha Kiswahili, kwa hoja kwamba Kiingereza ni "lugha ya soko". Hata hivyo, uchambuzi wa ulinganisho wa marobota ya kahawa ya Kilimanjaro unathibitisha kinyume chake: makampuni mawili yaliyotumia lebo vya lugha mbili (Kiswahili + Kiingereza) yalipokea oda nyingi zaidi katika soko la kanda la Jumuiya ya Afrika Mashariki, zikiongezeka kwa asilimia 18 kati ya 2022-2024, ikilinganishwa na kampuni zilizouza kahawa yenye lebo cha Kiingereza pekee. Taarifa hii inalingana na matokeo ya **[4]** nchini Ujerumani kwamba bidhaa zenye lugha mchanganyiko huchangia mauzo mazuri kwa sababu zinajenga uaminifu na kuheshimu utamaduni wa mnunuzi.

Kwa hivyo, hoja ya watoa-taarifa kwamba lugha za kigeni pekee "hudhoofisha utamaduni" ina mashiko matatu makuu. Kwanza, inathibitisha dhahania ya **[20]** kwamba lugha inayokosa uhalali wa wenyeji hugeuka kikwazo hatari. Pili, inafichua athari ya kitamaduni na kiafya, hakuna ufafanuzi wa viambato unaoeleweka, hakuna tahadhari zinazoeleweka. Tatu, inapinga dhana kwamba kiuchumi Kiswahili hakina nafasi, kwa sababu data zinaonesha vibandiko mchanganyiko huimarisha soko badala ya kulidhoofisha.

Yote haya yanapounganishwa yanaibua hitimisho muhimu: ili kulinda utamaduni wa Zanzibar na haki za wateja, ni lazima sera ya vifungashio itamke wazi kwamba Kiswahili kiwe lugha ya msingi, kusaisaidiwa na tafsiri sahihi za Kiingereza au Kiarabu inapobidi. Mwelekeo huo unalingana na mhimili wa *lugha-kama-rasilimali* wa **[20]** lugha ya taifa inajengwa, utamaduni unadumishwa na soko linapanuka kwa kuwepo daraja la kuaminika kati ya mtumiaji na mtayarishaji.

3.3.3 Matumizi ya Lugha za Kigeni Hushusha Hadhi ya Kiswahili

Hoja kuu ya kipengele hiki ni kwamba msongamano wa lugha za kigeni, hususan Kiingereza, katika vifungashio vya bidhaa zinazozalishwa na kusambazwa nchini Tanzania unadhoofisha hadhi ya Kiswahili na kupunguza mamlaka ya lugha ya taifa katika uwanja ambao unagusa moja kwa moja afya, uchumi na utambulisho wa wazawa:

> *"Kiswahili ndiyo uti wetu wa mgongo; tunapojaribu kusoma kibandiko tukazikuta zote kwa Kiingereza, tunahisi lugha yetu haifai tena, jambo linalotudunisha sisi na tamaduni zetu*"

Nukuu hii inafichua hisia za kudharauliwa wanazoibuka nazo watumiaji wanapolazimishwa kukabiliana na lugha za kigeni katika nyanja wanayoweza kuifahamu kwa urahisi kupitia Kiswahili. Maelezo haya yanaunga mkono moja kwa moja mhimili wa lugha kama tatizo katika Nadharia ya Mielekeo ya Upangaji wa Lugha ya **[20]** anaeleza kuwa lugha hujikita kuwa kikwazo pindi inapowekwa kwenye nafasi isiyoeleweka au isiyofikika kwa kundi lengwa la watumiaji. Katika muktadha wa Zanzibar, lugha za kigeni zinachukua nafasi hiyo ya kikwazo: zinazuia ufikivu wa taarifa zinazohusu uhifadhi, dozi, viambato na tahadhari na pia zinatuma ujumbe unaodhalilisha hadhi ya Kiswahili, ambacho ni nyenzo ya pamoja ya wananchi wote.

Mtoataarifa "S" aliyerekodiwa Kikwajuni alieleza:

> "*Kadri vifungashio vinavyokithiri kuandikwa kwa Kiingereza, tunafundishwa kimyakimya kuwa hakuna thamani kwenye Kiswahili".*

Kauli hii ya mtoaatarifa inaakisi usemi wa [12] kuwa chaguo la lugha kwenye vifungashio "huchora mpaka wa hadhi" kati ya lugha zinazokuzwa na zile zinazodunishwa. Uamuzi wa kiutawala wa kuweka Kiingereza mbele, licha ya sera ya kitaifa inayotambua Kiswahili kama lugha ya taifa, unaunda jeraha la kisaikolojia linalotafsiriwa na mtoataarifa kama "kudunishwa". Kwa kuzingatia mhimili wa *lugha-kama-haki*, hali hii ni ukiukaji dhahiri wa haki ya mtumiaji kupata taarifa kwa lugha anayoimudu, haki ambayo imezibwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR 1966, kifungu 27) unaolinda matumizi ya lugha za wachache au za wenyeji. Kiathari, ukosefu wa Kiswahili katika vifungashio si kero ndogo tu katika lugha bali ni kitisho cha usalama wa watumiaji. **[2]** aliripoti visa vya wazazi Dodoma walioandaa maziwa ya unga yaliyokwisha muda kwa sababu hawakuelewa kifungu cha '*expiry date'* kilichoandikwa Kiingereza pekee.

Katika mtazamo wa lugha-kama-rasilimali, kuporomoka kwa hadhi ya Kiswahili ni kuvuja kwa mtaji wa kijamii, kitamaduni na kiuchumi**. [3]** anakumbusha kwamba hadhi hutoa mwamko wa matumizi mapya ya lugha kitaifa, huku [**1]** akifafanua kuwa kadiri lugha inavyotumika katika sekta za thamani, ndivyo inavyoongeza utajiri wa kifikra na fursa za ajira kwa wazungumzaji wake.

Madai ya baadhi ya watetezi dhidi ya hoja hii yanadai "Kiingereza huvutia soko la kimataifa", hoja inayojibiwa na **[8]** kwamba mtaji wa lugha hupanda thamani ili mradi uhusike na walio wengi sokoni. Kwa Zanzibar", walio wengi" ni watumiaji wanaotegemea Kiswahili. Ukweli huu unaungwa mkono na ugunduzi wa [4**]** kwamba lebo mchanganyiko huongeza, badala ya kupunguza, ushindani wa kimataifa.

Kwa jumla, data za utafiti zimejenga mnyororo wa hoja unaodhihirisha kuwa nguvu ya lugha za kigeni kwenye leboo vya bidhaa ni mbinu ya "kunyamazisha" Kiswahili na kwa mlingano ule ule, kustawisha mazingira yanayovuruga utamaduni na kuhatarisha haki za mtumiaji. Hivyo, sera inahitajika kuagiza Kiswahili kama safu ya kwanza ya maelezo, ikisaidiwa na tafsiri sahihi za Kiingereza au lugha nyengine, ili kurejesha hadhi ya lugha ya taifa, kuimarisha usalama wa bidhaa na kutumia ipasavyo rasilimali ya lugha ya Kiswahili katika mzunguko wa uchumi na utamaduni wa Zanzibar.

3.3.4 Matumizi ya Lugha za Kigeni Yanatokana na Ukoloni

Matumizi ya lugha za kigeni, hasa lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa nchini Tanzania, yanatokana na mabaki ya athari za ukoloni ambazo bado zinaathiri sera, mitazamo na maamuzi ya kisera kuhusu lugha. Muktadha huu unaonesha kuwa, lugha ya Kiingereza haijatamalaki tu kwa sababu ya umuhimu wake wa sasa katika nyanja za kimataifa, bali kwa sababu ilihalalishwa na kuimarishwa na wakoloni kama chombo cha mamlaka, biashara, elimu na mawasiliano ya kiutawala.

Katika utafiti huu, mtoataarifa mmoja kati ya watoataarifa sita waliopinga matumizi ya lugha za kigeni katika vifungashio alieleza kuwa:

> "*Kutumia lugha za kigeni husussan lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania, bila ya shaka kunatokana na athari za ukoloni*". [13]

Kauli hii inafichua mtazamo mpana kwamba uamuzi wa kutumia Kiingereza katika mawasiliano ya bidhaa si tu uamuzi wa kibiashara, bali ni urithi wa uhusiano wa kiukoloni unaoendelea kuathiri sera na maamuzi ya kisera hadi leo. Mtoataarifa amefafanua kuwa:

> *"Watayarishaji wa bidhaa hufanya hivyo kwa kisingizio kuwa, Zanzibar ni eneo la utalii. Hivyo, hutumia lugha za kigeni ili kukuza soko la biashara zao*.[14]

Hii inaonesha kuwa hata mazingira ya kibiashara yanayotegemea utalii yanachochea utegemezi wa lugha ya Kiingereza kwa misingi ya kihistoria na kisaikolojia inayodunisha lugha ya wenyeji, Kiswahili.

Hoja hii inashabihiana na mtazamo wa **[20]** kupitia nadharia ya Mielekeo katika Upangaji wa Lugha. **[20]** anaeleza kuwa lugha huweza kutazamwa kwa mitazamo mitatu: lugha kama tatizo, lugha kama haki na lugha kama rasilimali. Katika muktadha huu, matumizi ya Kiingereza pekee katika vifungashio vinaweza kuchambuliwa kupitia lugha kama tatizo, kwani havifanikishi mawasiliano sahihi kwa watumiaji wazawa. Vilevile vinaakisi mitazamo hasi ya kihistoria ambapo lugha ya Kiswahili haijathaminiwa ipasavyo licha ya kuwa rasilimali ya kiutamaduni, kijamii na kiuchumi.

[21] alifanya uchambuzi linganishi kati ya Pakistan, Kenya na Malaysia na kubainisha kuwa ukoloni wa Kiingereza uliacha urithi wa lugha katika sera za elimu, biashara na sheria. Nchini Zanzibar, hali hii imepelekea lugha ya Kiingereza kutumika katika maeneo mengi ya maisha ya

[13] Mahojiano, mtoa taarifa "T" kutoka mtaa wa *Mwembeladu*, *15/08/*2024

[14] *Maelezo hayo yametolewa na mtumiaji "X" wa bidhaa aliyefanyiwa mahojiano na mtafiti. Tarehe* 18/09/2024.

kisasa licha ya ukweli kuwa Kiswahili ndicho chombo kikuu cha mawasiliano kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi.

Kadhalika, [15] anaeleza kuwa, lugha za wakoloni zinaendelea kutawala katika shughuli rasmi za Afrika kutokana na historia ya ukoloni ambayo haikupingwa kisera baada ya uhuru. **[15]** amesema:

> "*Shule zetu hufundisha Kiingereza kama lugha ya maarifa, Kiswahili kama mapambo. Hii ni dhana iliyozalishwa na wakoloni na inaendelea kuishi*".

Katika muktadha huo, matumizi ya lugha ya Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa huendeleza hali ya kisiasa ya "kutegemea lugha ya mkoloni" kama nembo ya usasa au maendeleo, huku Kiswahili kikiachwa pembeni kama lugha ya 'kawaida' ya nyumbani.

Kwa mujibu wa **[27]** ushawishi wa Kiingereza duniani kote haukutokana tu na uzuri wa lugha hiyo bali ni matokeo ya sera makini za kikoloni zilizolenga kuenea kwa utamaduni wa Kiingereza kupitia elimu, utawala na biashara. Pia, anaeleza kuwa mpango wa muda mrefu wa Mwingereza ulikuwa ni kufanya lugha yake kuwa kiungo muhimu katika soko la kimataifa na mawasiliano ya kitaifa ndani ya koloni zake.

[29] wanaongeza kuwa, kusambaa kwa lugha ya Kiingereza kulikuwa na malengo ya kimkakati ya kueneza utawala wa kiutamaduni na kiuchumi wa mataifa ya Magharibi. Wanasema kuwa, matumizi ya lugha hii kama chombo cha biashara, diplomasia na teknolojia si tu kwa sababu ya "ubora wake wa kimantiki" bali kwa sababu ya nguvu ya kiuchumi na kijiografia ya waliokuwa na lugha hiyo.

Katika utafiti huu, hoja ya kwamba "Zanzibar ni eneo la utalii" imetajwa kama kichocheo cha utegemezi wa lugha za kigeni katika vifungashio. Hii inahitaji kuchambuliwa kwa kina. Ni kweli kuwa Zanzibar hupokea watalii kutoka mataifa mbalimbali, lakini bado ni Wazanzibari ndiyo wanunuaji wakuu wa bidhaa nyingi za kila siku. Hivyo, hoja ya kutumia lugha za kigeni kwa ajili ya watalii inakosa mashiko

Katika muktadha wa lugha kama haki, kama anavyopendekeza **[28]**, watumiaji wa Tanzania wana haki ya kupata maelezo ya bidhaa kwa lugha wanayoimudu, Kiswahili. Kitendo cha kutumia lugha ya Kiingereza pekee katika vifungashio kinapingana na msingi wa ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi na haki ya maarifa kuhusu bidhaa wanazotumia.

Aidha, [10**].** anaeleza kuwa, lugha za wakoloni zilibeba hadhi iliyozalishwa kwa nguvu ya utawala, elimu na dini. Anasisitiza kuwa, lugha hizo zimebakia kama alama ya mamlaka katika nchi nyingi za Afrika, ambapo wenye lugha asilia huziona lugha zao kuwa duni na zisizofaa kwa shughuli za kimataifa.

Hoja hizi zote zinaleta mwangwi wa msingi wa hoja ya mtoataarifa ambaye anahimiza kuwa, kama kweli Kiswahili kinakua duniani, basi Zanzibar na Tanzania kwa ujumla zinapaswa kuwa mfano wa kwanza wa kulikuza kupitia njia halisi kama vile kutumia Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa zinazotengenezwa nchini.

Hata hivyo, [**17]** anapinga hoja ya kwamba matumizi ya lugha za kigeni ni mabaki ya ukoloni kwa kueleza kuwa, hata mataifa yasiyotawaliwa hutumia Kiingereza kwa hiari kama lugha ya biashara

na kimataifa. Ingawa hoja yake inatoa upana wa mjadala, bado inapuuzia ukweli wa kimuundo kuwa Kiingereza kilipandikizwa kwa nguvu kama lugha ya elimu, mamlaka na maendeleo katika nchi za Kiafrika na athari zake bado zinatawala sera nyingi za lugha hadi leo.

Kwa kuhitimisha, hoja ya kwamba matumizi ya lugha za kigeni, hasa Kiingereza katika vifungashio vya bidhaa nchini Tanzania ni mabaki ya ukoloni, inajengwa kwa msingi wa kihistoria, kijamii na kiutamaduni. Ni wazi kuwa urithi wa ukoloni bado unaathiri uchaguzi wa lugha katika sera na shughuli za kila siku. Ili kulinda hadhi, utambulisho na haki za watumiaji wenyeji, ni muhimu sera za lugha zihamasishe matumizi ya Kiswahili katika vifungashio vya bidhaa, ili kuondokana na minyororo ya kihistoria na kukuza uhuru wa kweli wa utamaduni na uchumi wa Tanzania.

4.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imefafanua mitazamo ya watumiaji wa bidhaa juu ya matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa. Matokeo yameonesha kuwa, watumiaji wa bidhaa wanathamini suala la utumiaji wa lugha katika vifungashio vya bidhaa. Aidha, watumiaji 14 kati ya 30 waliohojiwa wamedai kuwa vifungashio vya bidhaa za chakula vitumie Kiswahili na lugha nyingine za kigeni ili kuendana na soko la kimataifa na ushindani wa kibiashara katika soko la kimataifa. Matumizi ya lugha katika vifungashio vya bidhaa za chakula lina athari kubwa kiuchumi na kijamii. Hivyo, ni vyema kwa wazalishaji wa bidhaa kutumia lugha zinazofahamika na jamii ili upatikanaji wa haki ya lugha ufikiwe kikamilifu. Aidha kwa bidhaa zinazouzwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ni vyema kwa wazalishaji wa bidhaa licha ya kuzingatia lugha za kigeni pia watumie lugha ya Kiswahili kwa vile ni lugha ambayo inafahamika zaidi nchini Tanzania. Hatua hii itasaidia watumiaji wa bidhaa kuzitumia kwa uhakika, pamoja na kupunguza madhara ya kiafya kwa watumiaji. Kulingana na matokeo ya uchunguzi, makala hii inapendekeza kuwa: Waandaaji wa Mwongozo wa Usajili wa Chakula Zanzibar wazingatie hadhi ya lugha ya Kiswahili katika upangaji wa lugha katika vifungashio vya bidhaa zinazouzwa nchini.
Pia watafiti wanapaswa kuchunguza madhara ya kiafya kwa watu waliotumia bidhaa pasi na kufahamu maelekezo yaliyoandikwa katika bidhaa.

Marejeleo

[1]Ababaker, E. A. (2013). *Maendeleo ya lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu: Mtazamo wa kilughawiya jamii*. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

[2]Abdallah, S. (2018). Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika bidhaa za watoto: nchi Tanzania, yaliyokuwemo na yasiyokuwemo. *Jarida la Mwanga, 2*(2), 1–12. Katika https://journals.mu.ke/ index.php/mwl/article/ view/88.

[3] Bianco, J. L. (2016). *Language policy and planning*. Multilingual matters. https://doi.org/10.21832/9781847692849-008.

[4] Bourdieu, P. (1997). Language and Symbolic Power (J. B. Thompson, Ed.). Harvard University Press.

[5] Charinsarn, A., & Wagner, U. (2020). What language should be displayed on product packaging? *Journal of International Consumer Marketing, 33*(5), 1–18. https://doi.org/10.1080/ 08961530.2020 .1741748

[6] Chimerah, R. M. (1998). Kiswahili: Past, present and future horizons. Nairobi: Nairobi University Press.

[7] Han-Chiang Ho, C., Lim Chiu, C., Jiang, D., Shen, J., & Xu, H. (2019). Influence of language of packaging labels on consumers' buying preferences. *Journal of Food Products Marketing*. https://doi.org/ 10.1080/10454446.2019.1572562

[8] Hornikx, J., & Starren, M. (2006). Linguistic landscapes and the representation of languages on product packaging. Journal of Applied Communication Research, 34(1), 95–112. https://doi.org/10.1080/ 00909880500420276

[9] Hult, F. M., & Hornberger, N. H. (2016). Revisiting orientations in language planning: Problem, right, and resource as an analytical heuristic. *Bilingual Review, 33*(3), 30–49.

[10] Institute of Export of America. (2022). International labeling guidelines: Language and Legal Compliance in Packaging. Retrieved from https://www.export.org.

[11] Kiprotich, P. J. (2017). Nafasi ya lugha katika kukabiliana na changamoto za kijamii, kiuchumi na kisiasa Afrika. *Jarida la UDSM*.

[12] Lodhi, A. Y. (1992). *The role of Kiswahili in the context of Zanzibar*. Paper presented at the international conference on history and culture of Zanzibar.

[13] Maack, V. H., & Schwenk, J. (2016). Effects of multilingual product packaging on product attitude, perceived quality, and taste perceptions. In K. Diehl & C. Yoon (Eds.). *Advances in advertising research* (Vol. 6, pp. 351–363). Springer. https://doi.org/10. 1007/978-3-658-10558-7_27

[14] Mwinyikombo, F. (2021). Athari za utandawazi kwa lugha asilia barani Afrika. Journal of African Languages and Literature, 13(2), 78–94.

[15] Ofisi ya Taifa ya Takwimu. (2021). Takwimu za maendeleo ya jamii Tanzania Bara 2021. Dodoma: Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

[16] Ofisi ya Takwimu ya Taifa. (2024). Ripoti ya hali ya uchumi ya taifa 2024. Dodoma: Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

[17] Pattison, E. (2018, May 3). Why language is crucial to succeeding in new markets. *Marketing Week*. https://www.marketingweek. com

[18] Powell, R. (2002). Language planning and the British Empire: Comparing Pakistan, Malaysia and Kenya. *Current Issues in Language Planning, 3*(3), 205–279. https://doi.org/10.1080/ 1466420020866 8041.

[19] Rais, A. S., Onyango, J., & Mbaabu, I. (2022). Tathmini ya uamilifu wa kiswahili nchini Uganda. *East African Journal of Swahili Studies, 5*(1), 73–83. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1. 641

[20] Ruiz, R. (1984). Orientations in language planning. *NABE Journal*, 8(2), 15–34. https://doi.org/10.1080/08855072.1984.1066 8464.

[21] Run, E. C. D., & Chin, S. F. (2006). Language use in packaging: The reaction of Malay and Chinese consumers in Malaysia. *Sunway Academic Journal, 3*, 133–145.

[22] Shangkuan, S. (2022). Consumer culture and language preference in packaging: Evidence from East Asia. *Journal of Marketing and Language*, 29(1), 51–70.

[23] Shitemi, N. (2011). Kubidhaisha lugha kama sarafu ya kiuchumi na kijamii. *Mhadhara wa Uzinduzi wa Taaluma ya Kiswahili, Moi University*.

[24] Shohamy, E. (2006). Language policy: Hidden agendas and new approaches. Routledge.

[25] Simkus, J. (2022). Cluster sampling: Definition, method and examples. *Simply Psychology*. https://www.simplypsychology.org/ cluster-sampling.html.

[26] Thomas, L. (2023). Cluster sampling: A simple step-by-step guide with examples. *Scribbr*. https://www.scribbr.com/methodology/ cluster-sampling.

[27] Tsuda, Y. (2008). English hegemony and English divide. *China Media Research, 4*(1), 97–103.

[28] Whiteley, W. H. (1969). Swahili: The rise of a national language. Methuen & Co.

[29] Zeng, J., & Yang, Y. (2024). English language hegemony: Retrospect and prospect. *Humanities & Social Sciences Communications, 11*(28). https://doi.org/10.1057/s41599-024-02821-z